



## DCB Commercial Bank Plc

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MOJA WA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa ishirini na moja wa wanahisa wa DCB commercial bank Plc, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 17 Juni 2023, katika ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar-es-Salaam, kuanzia saa tatu kamili (3:00) asubuhi.

#### Agenda

1. Kufungua mkutano mkuu wa mwaka
2. Kuridhia agenda ya Mkutano Mkuu wa ishirini na moja wa mwaka
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 20 wa mwaka uliofanyika tarehe 11 Juni 2022
4. Kupokea na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 20 wa mwaka
5. Kupokea na kuridhia
  - 5.1 Taarifa ya wakurugenzi ya mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2022
  - 5.2 Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2022
  - 5.3 Taarifa ya mkaguzi huru ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2022
6. Kupokea na kuridhia Mabadiliko ya Vifungu vya Katiba ya Kampuni
7. Kupokea taarifa ya Kuisha kwa muda, Kuongeza muda na uteuzi wa wajumbe wa bodi
8. Kuteua mkaguzi huru wa hesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2023
9. Kupokea na kuridhia pendekezo la malipo ya ada kwa wajumbe wa bodi
10. Kupokea taarifa ya gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2022
11. Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa ishirini na mbili
12. Mengineyo
13. Kufunga mkutano

#### MAELEZO

1. Mwanahisa atakayehudhuria Mkutano Mkuu anatakiwa kujigharamia mwenyewe na aje na hati ya hisa iliyotolewa na Soko la Hisa la Dar-es-Salaam pamoja na kitambulisho chake cha kupiga kura au cha taifa au hati ya kusafiria.
2. Mwanahisa anayestahili kuhudhuria na kupiga kura lakini akashindwa kuhudhuria kikao, anaweza kuwasilisha Jina la Mbadala wake (Proxy) ambayo inaonyesha kura alizopiga katika kila agenda kwa Katibu wa benki kabla ya saa 08:00 mchana Alhamisi ya tarehe 15 Juni 2023 katika ofisi za Makao Makuu zilizoko jengo la DCB, Magomeni Mwembechai au kwa barua pepe kupitia [shareholders@dcb.co.tz](mailto:shareholders@dcb.co.tz) au [info@dcb.co.tz](mailto:info@dcb.co.tz). Kwa makampuni, fomu inapaswa kuwa katika lakiri ya kampuni mwanahisa.
3. Kufungwa kwa orodha (Register) ya wanahisa - tarehe 12 Juni 2023
4. Mapendekezo ya wanahisa yawasilishwe kwenye ofisi za makao makuu zilizoko jengo la DCB Magomeni Mwembechai au kwa barua pepe kabla ya saa 8.00 mchana siku ya Alhamisi tarehe 15 Juni 2023.
5. Vitabu vyenye taarifa ya hesabu ya mwaka 2022 pamoja na fomu ya mwakilishi mbadala (proxy) vitapatikana ofisi za makao makuu zilizoko jengo la DCB, Magomeni Mwembe chai na katika matawi yote na ofisi za madalali wa Soko la Hisa la Dar-es-Salaam na kwenye tovuti ya benki [www.dcb.tz](http://www.dcb.tz) kuanzia tarehe 12 Juni 2023.

KWA IDHINI YA BODI,  
Regina Mduma  
Katibu wa Kampuni  
Mei 2023.